# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS – TAMISEMI

**Namba za simu:** *Shule ya Sekondari* **KIMANI,**

**S.L.P. 28001,**

**Mkuu wa Shule: +255 624 753 492**

**Makamu Mkuu wa Shule 0621600705** **KISARAWE.**

**Patron: +255 756351158**

**Baruapepe: kimaniss2020@gmail.com**

**APRIL, 2024**

---

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi……………………………………………….**
**S.L.P. …………**
**………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIMANI HALMASHAURI YA KISARAWE MKOA WA PWANI MWAKA 2024.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano mwaka 2024 katika shule hii tahasusi ya ………… Shule ya Sekondari Kimani ipo umbali wa Kilometa 1.5 Kaskazini mwa mji wa Kisarawe. Njia rahisi ya kufika Kimani Sekondari ni kupanda mabasi(Dala Dala) yaendayo Gongo La Mboto Jijini Dar es Salaam. Shuka Gongolamboto mwisho. Nauli ni sh.500/= hadi 700/= au 200/= mwanafunzi kutegemea stendi utakayopandia. Ukifika Gongolamboto panda magari yanayokwenda Kisarawe (nauli ni sh.550/=) au 200/= mwanafunzi. Utashuka mwisho wa gari Stendi ya Kisarawe Mjini ambapo utapanda bajaji (sh.2000/=) au pikipiki(sh.1,000/=) kuelekea shuleni.

   **Muhula wa masomo unaanza tarehe 01/07/2024**
   **Hivyo, mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 30/06/2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 30/07/2024.**

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**
   2.1 Sare ya shule
   a) Sare ya shule hii ni suruali mbili (2) "Dark Blue" zenye marinda mawili kwa mbele, mfuko mmoja mmoja kulia na kushoto; na mfuko mmoja wa nyuma upande wa kulia. Iwe na pindo kwa chini, wala isiwe fupi ya kubana (modo hazikubaliki) (Mwanafunzi anaweza kuzipata karibu na shule kwa kufanya mawasiliano mapema).
   b) Shati mbili (2) nyeupe zenye mikono mirefu (Mwanafunzi aje nazo).
   c) Fulana (T-shirt) zenye nembo ya shule. Zinapatikana karibu na shule
   d) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino/vidani vifupi.
   e) Soksi jozi mbili(2) nyeusi za shule (aje nazo).
   f) Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali(aje nao).
   g) Tai pea mbili dark blue ndefu. Zinapatikana karibu na shule
   h) Sweta la "dark blue" lisilokuwa na maandishi. linapatikana karibu na shule

i) Nguo za kushindia (shamba dress) ni suruali mbili nyeusi ziwe zenye marinda mawili mbele kila upande na t-shirt rangi ya bluu (t-shirt zinapatikana karibu na shule
j) Mwanafunzi aje na viatu vya michezo rangi yoyote (ngozi au raba) na kaptula au tracksuit ya blue isiyo na maandishi. Tracksuit inapatikana karibu na shule.

**2.2 Michango mbalimbali**

a) Michango ilipwe kwenye akaunti ya shule Na.**21401100020** NMB (Jina la akaunti ni: **Kimani Secondary School**). **TAFADHARI ANDIKA JINA LA MWANAFUNZI (SIO MZAZI/MLEZI) kwenye Bank Pay in Slip.** (Nakala halisi iletwe shuleni, na mzazi/mlezi apige photocopy kubaki na nakala ya kumbukumbu ya malipo yake).
b)

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

(i) **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka
(ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatishwa)
(iii) Scientific calculator kwa wanafunzi wa tahasusi ya PCM.
(iv) Godoro la inchi 2.5 jipya .
(v) Mashuka pair 2 (Light blue), mto na foronya yake 1 (Light blue) na chandarua chenye dawa (cha futi 3x6 pembe nne rangi ya blue/light blue).
(vi) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe). Vyombo vya plastiki haviruhusiwi. Shule haina utaratibu wa kutoa chakula maalumu (special diet) kwa mwanafunzi mwenye matatizo!
(vii) Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
(viii) Nguo za ndani za kutosha
(ix) Fagio za chooni 1 (hard broom) na fagio1 la ndani (soft broom) kwa kila mwanafunzi wa PCM.
(x) Fagio 1 la nje "chelewa" lenye mpini mrefu na squeezer 1Kwa kila mwanafunzi wa HGL
(xi) Panga na kwanja kwa kila mwanafunzi wa HGLi
(xii) Madaftari/counter mbili kwa kila somo (quire 3 au 4); kalamu na penseli za kutosha, mkebe wa Hisabati, Laboratory coat, stop watch na thermometer kwa tahasusi ya PCM.
(xiii) Folder file 1 kwa ajili ya kuhifadhi taarifa muhimu shuleni.
(xiv) Result Slip ya Kidato cha Nne (CSEE) halisi na nakala moja. Cheti cha kuzaliwa(Birth Certificate) halisi na nakala moja. Siyo Hati ya Uthibitisho wa Kuzaliwa (Affidavit).Cheti cha Kumaliza Kidato cha Nne (School Leaving Certificate) halisi na nakala.

## Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule.**

**3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i) Wizi.
ii) Kutokuhudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi au na mtu yeyote yule, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi) Kusuka nywele kwa mtindo wowote ule.Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii) Kufuga ndevu.
viii) Ulevi au unywaji pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
ix) Uvutaji sigara.
x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja (ushoga), kuoa au kuolewa.
xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
xiii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xiv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xv) Kudharau Bendera ya Taifa.
xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xvii) Uhalibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xviii) Kwenda kwenye vigodoro mchana au usiku.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.
b) Fomu ya Maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na kulipa michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Picha nne (4) za Wazazi/Walezi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

5. **Tafadhari soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.**

**Saini ya Mkuu wa Shule**: …………………………

**Jina la Mkuu wa Shule**: JUMANNE MARCO KINGU

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**: …………………………..

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE**
**SHULE YA SEKONDARI KIMANI**
**FOMU YA TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. Jina lako kamili ………………………………………………………………………
2. Kidato ulichojiunga hapa shuleni ……………………… Tahasusi ……………
3. Jina la mzazi /mlezi ……………………………………………………………………
   Anuani yake ………………………………………………………………………………
   Simu yake ya Mkononi …………………………… Ya ofisini ……………………
   Kazi yake …………………………………………………………………………………
4. Mahali ulipozaliwa:
   i) Mkoa ………………………………… Wilaya ……………………………
   ii) Tarafa ………………………………… Kata ………………………………
   iii) Kijiji /Mtaa…………………………………………………………………
   iv) Tarehe ya kuzaliwa ………………………………………………………

5. Mahali unapoishi sasa ………………………………………………………………
   Anuani yako ……………………………………………………………………………
   Nambari za simu ………………………………………………………………………

6. Dini/Dhehebu lako ……………………………………………………………

7. Unaishi na baba tu/ mama tu/ wazazi wote/ mlezi ……………………………

8. A) Jina la Shule za Msingi ulizosoma:
   i) Shule ya Msingi ……………………… Anuani …………………….
   ii) Shule ya Msingi ……………………………… Anuani ………………
   B) Jina la Shule za Sekondari ulizosoma:
   i) Shule ya Sekondari uliyoanzia …………… Anuani………………
   ii) Shule ya Sekondari uliyomalizia………… Anuani ………………
9. Michezo unayocheza:
   a) ……………………………………………………………………………………
   b) ……………………………………………………………………………………

10. Vyama vya kujifunza ambavyo wewe ungependa kuwa mwanachama: Scout na Mazingira, FEMA, PCCB, School Magazine ………………………………
11. Je? Unao ulemavu wowote? (Ndiyo/Hapana)………………………………
    Kama Ndiyo, taja aina ya ulemavu ……………………………………………
    **N.B.:** Mazingira ya shule si rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu!

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE**
**SHULE YA SEKONDARI KIMANI**

**FOMU YA UTHIBITISHO**

Fomu hii ijazwe na mzazi/mlezi wa mwanafunzi katika sehemu zake na irudishwe shuleni ikiwa imeambatanishwa na picha ya mzazi/mlezi.

Mimi (Jina kamili) ………………………………………………………………………
mzazi/mlezi wa mtoto wangu (Jina la mwanafunzi)……………………………
ninafurahi kupata nafasi aliyochaguliwa mtoto wangu. Nimeona, nimesoma, nimeelewa na kukubali masharti yote yanayohusu mtoto wangu kujiunga na Shule ya Sekondari Kimani. Nitahakikisha ninampa mahitaji yote yanayotakiwa mtoto wangu ili aripoti muda uliopangwa, na nitakuwa tayari kushirikiana na walimu wa shule ya Kimani katika malezi na taaluma yake muda wote atakaokuwa shuleni hapo ili aweze kufikia malengo yake na Taifa kwa ujumla.

Saini ya Mzazi/Mlezi:……………………………………………………….

Jina la Mtendaji wa Kijiji/Mtaa ……………………………….. Simu: ……………

Saini ya Mtendaji wa Kijiji/Mtaa na Mhuri: ………………………………………….

**TAMKO LA MZAZI/MLEZI:**
Mimi ……………………………………………………………………………………… …… Mzazi/mlezi wa mwanafunzi………………………………………………… wa kidato cha TANO; kwa akili zangu timamu, nakiri kwamba yaliyoandikwa hapo juu kwenye fomu ya Taarifa za Mwanafunzi na fomu ya Uthibitisho ni sahihi.

**SAINI YA MZAZI/MLEZI : ………………………….. Simu: ……………………**

PICHA NO.1 PICHA NO.2 PICHA NO.3 PICHA NO.4

**MZAZI/MLEZI** **NDUGU-1** **NDUGU-2** **NDUGU-3**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE**
**SHULE YA SEKONDARI KIMANI**

**FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA**

(Request for Medical Examination)
This form is to be completed by a Medical Officer.
Name of pupil: ……………………………………… Age: ……… Sex: …….
The above named has been examined in respect of:

(a) **STOOL**
…………………………………………………………………………………

(b) **URINE**
………………………………………………………………………………….

(c) **CHEST**
…………………………………………………………………………………

(d) **BLOOD**
………………………………………………………………………………..

(e) **EYES**
……………………………………………………………………………………

(f) **EARS**
……………………………………………………………………………………

(g) **HEART**
…………………………………………………………………………………

(h) **STOMACH ULCERS**
…………………………………………………………………

(i) **OTHERS**
……………………………………………………………………………….
……………………………………………………………………………………….

I am satisfied / not satisfied that the above named student is physically and mentally fit to pursue further studies in Secondary School.

……………………………………………………………………
**SIGNATURE and ( Official Stamp )**
**DATE: …………………………………**

…………………………………………
**DESIGNATION**
**STATION:………………………………….**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/ MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule …….............0756234291 AU 0624753492.**
- **Makamu Mkuu wa Shule ….0621600705 AU 0765487525**
- **Mwandamizi Taaluma ………0620204018**
- **Mwandamizi Malezi …………0766343639.**

**VIFUATAVYO NI BAADHI YA VITABU VINAVYOTUMIKA SHULENI**

Mwanafunzianashauriwakununuavitabukulingananamasomoyakekwakufuatamchanganuooufuatao.

**CHEMISTRY**

1. Modern's ABC of Chemistry by Dr. s. Jauhar (2017-2018) for class XI & XII part I & II

2. Essentials of Physical Chemistry class XI & XII by Chand

3. Advanced Physical Chemistry by NgaizaLusima (2014)

4. Conceptual Chemistry for Class XI by S.K JAIN

5. Comprehensive Chemistry volume I class XII by Dr. N.K. Verma, S.K. Khanna& Dr. B. Kapila

6. Advanced Organic Chemistry by ArunBahl, S. Chand

**GENERAL STUDIES**

1.Understanding General Studies For Advanced level (5&6) by JoannesBigirwamungu&Sospeter M. Deogratius

2.General Studies Alive (5&6) by ZistiKamili (2017)

3.General Studies Notes: Current syllabus Approach form 5&6 by NyambariNyangwine, G.M Zombwe, Godfrey Mshiu& James Egino

**HISTORY**

1.Advanced Learning World History by IdrisaMsuya book 1 & 2

2.Essentials in Advanced level History paper 1 & 2 by SalehYasin

3.Advanced Level History 1 & 2 by K. Shibitali

4.Medieval Ages paper 2 by M Mavunde Mohamed, Oxford University Press

**ADVANCED MATHEMATICS**

1. Advanced Mathematics for Advanced Secondary Schools Form V by Septine I. Sillem (2015)

2. Advanced Mathematics for Advanced Secondary Schools Form VI by Septine I. Sillem (2015)

3. Conceptual Advanced Mathematics For Secondary Schools Form V by P. L. Mayombya

4. Conceptual Advanced Mathematics For Secondary Schools Form VI by P. L. Mayombya

**GEOGRAPHY**

1.Integrated Approach in Geography by David Waugh (2009) 3rd edition

2.A Comprehensive  Approach in Physical Geography by D.T. Msabila (2018)

3.Practical Geography by ZistiKamili 2nd Edition 2016

4.Complementary Physical Geography for secondary school by O. Mpalaki& F. Lighuda

5.Affordable Edition for Advanced learners by ZistKamili

**ENGLISH LANGUAGE**

1.Advanced level English Language 1 by Ndambo, NNP Publishers

2. Advanced English Language form 5&6 by James John, Oxford university press

3. English language for secondary school, language and use form 5&6 by TIE

4. Advanced level English language form 5&6 by NicholousAsheli

5. Oxford Advanced learners Dictionary by Oxford university press

6. Betrayal in the city by Francis Imbunga, East African Education publishers

7. The Beautiful ones are not yet Born by AyiKweiArmah. Heinemann Educational Publishers

8. A man of the people by Chinua Achebe. Heinemann Educational Publishers

9. An Enemy of the people by Henrick Ibsen. East African Educational Publishers

10. Black Mamba by John Ruganda

11. I will Mary when I want by NgugiwaThiong'o and Ngugi wa Mirii His Excellency The head of State by Danny Safo. Macmillan Publishers limited

12. Selected Poems by TIE

13. The Wonderful Surgeon and other Poems by Charles Mloka

14. A Season of Waiting by David Omowale. East African Educational Publishers

**PHYSICS**

1.Physics for Advanced level secondary schools, students book Form five by TIE

2. Physics for Advanced level secondary schools, students book Form six by TIE

3.Principles of physics for class XI, V.K Mehta, S. Chand

4. Principles of physics for class XII, V.K Mehta, S. Chand 5. Modern ABC of physics for class XI part I & II by Satish K. Gupta

6. Modern ABC of physics for class XII part I & II by Satish K. Gupta